P320/3
FASIHI YA KISWAHILI
Paper 3
Nov./Dec. 2025
3 hours

# UGANDA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

## Uganda Advanced Certificate of Education

FASIHI YA KISWAHLI

**Karatasi ya Tatu**
**(Riwaya)**

Saa Tatu

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

*Karatasi hii ina Sehemu* **nne**; **A, B, CH** na **D.**

*Mtahiniwa anapaswa kujibu maswali* **matatu** *kwa jumla; swali moja* **lazima** *litoke sehemu* **A** *na mengine mawili yachaguliwe kutoka sehemu* **B, CH** *na* **D.**

*Mtahiniwa asichague maswali zaidi ya* **moja** *kutoka sehemu moja.*

*© 2025 Uganda National Examinations Board*

## SEHEMU A

**SAID A. MOHAMED:** *Utengano*

**1.** 'Hakuna mwenye mdomo nyumba hii?' Maksuudi aliwageukia watumishi huku akizungusha bakora yake katika hewa. Kila mtu alikuwa katiwa maji. Wote waliufyata, Biti Kocho tu ndiye aliyejikazakaza. Hofu ilimtawala kila mtu, ikawanyweza walionywea, waliorejea, na waliobaki waliganda hapo hapo kama waliogongomelewa misumari. Lakini hapana aliyethubutu kujibu. Kwa hakika hakukuwa na jibu. Na kwa dakika hii, nani ambaye angalithubutu kusema mbele ya unyago wa bomba na Mti-mafuta?

Kimya kikaendelea kutawala.

'We we, we, we, we paka, we mwanaharamu,' Maksuudi alimgeukia tena Tamima. 'Wassahi nitakupiga leo, nikubakishe kope tu.'

Kimya chengine.

'Utasema husemi?'

'Nitakula nyama mbichi mimiiiiii,' Maksuudi alipiga kelele na kutikisa bakora yake hewani. Tamima huku akitetemeka, alirudi nyuma. Wote waliokuwepo walimeza pumzi moto.

'Maimuna yu wapi naseeeemaaaa. Ilikuwaje? Alaa, ndiyo mambo yako haya? Nikiondoka mimi wewe hutawala enn? Unamtorosha mwanangu na wewe mwenyewe unajiuza siyo? Yuko wapi Maimunaaaa?' Maksuudi ilimtoka bakora ambayo ilianguka juu ya kichwa cha Tamima. Tamima alipiga usiyahi mkubwa akaanguka chini. Muda ulipita. Maksuudi alihema kwa ghadhabu na Tamima aligaragara. Baadaye Tamima alipopata upumzi, alitupa mkono pale alipopigwa bakora. Damu ilikuwa ikimchururika.

Biti Kocho aliruka pale alipokuwa kasimama akawa anamwendea Bi Tamima, lakini Maksuudi alimtua, 'Eeeee, e-e-e-e, usisogee hapa. Usichezee moto!

Wakati huu, kati ya watumishi wote, hapana aliyebaki hapo, zaidi ya Biti Kocho na Fikirini ambaye kwa woga wake alijitahidi kuubandua mguu, lakini haukubanduka.

'Labda dharuba hiyo itakuamsha kidogo na kukuweka tayari kujibu masuala yangu.'

**Maswali:**

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (*Alama 08*)

(b) Tambua sifa za Maksuudi kama zinavyodhihirika katika dondoo hili. (*Alama 06*)

(c) Chambua mbinu za lugha zinazotumiwa na mwandishi katika dondoo hili kuwasilisha ujumbe. (*Alama 06*)

(d) Fafanua maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (*Alama 06*)

(e) Eleza hisia zinazoibuka kutokana na dondoo hili. (*Alama 04*)

(f) Donbdoo hili lina mafunzo gani kwa msomaji? (*Alama 04*)

**MOHAMED S. MOHAMED**: *Kiu*

**2.** "Kimekuleta nini huku?" alimkaripia, mknono wake mmoja ungali kiunoni mwa kile kisura ambacho sasa kilijisogeza zaidi karibu na Idi na kumwekea mkono begani huku kikimtazama Bahati kwa kumbeza.

"Nani yule darl…?" kiliuliza kisura, sauti yake ikijikokota, yenye dharau, legevu, nyororo.

"Huyu ndiye yule paka wangu niliyekwambia nafuga, lakini ngojea darl … nitamwondoa sasa hivi."

Bahati alitaka kuja juu, kutenda alilojia, lakini hakuwa na nguvu. Baada ya kumwita Idi kwa jina lake, alijiona bubu na kapooza. Alisimama tu pale mbele yao, tuli kama bendera shwarini na kuwakodolea macho, mwili wake ukaganda kama pande la barafu. Alimtazama yule mshindi wake na akamwona kama shetani mzuri; yeye mwenyewe akajihisi dhaifu, mdogo, mbaya wa kutupwa. Alimwona mumewe, Idi, anamjia, uso wake umejaa chuki na hasira. Akamsikia anamkemea na kumwinga: "Kimekuleta nini huku? Toka! Toka! Tokomea!"

Bahati aligeuka kama sanamu lililotiwa ufunguo akashika njia, na huko-o-mbele huko, ufunguo ukamalizika, akaanguka chini ya mti. Akalia … akalia … akalia … kitambo kirefu. Mwishowe, kama yale machozi yalimkosha akili yake, alijizoazoa akakaa na kuegemea shina la mnazi. Kwa mbali sasa akizisikia ghasia za nyumbani kwake. Akavuta fikira. Akakusanya nguzu zake zote na kuyawaza yale yaliyokwishatokea. Alitanabahi kuwa hakufanya kitu. Alijifedhehi tu. Sasa lazima atende jambo. Lazima yaishe wakati ule ule. Hatayarimbikiza tena. Hatakwenda kumdai Idi au kumwingilia, au kuyarejesha yaliyopita. Hatagombana. Atakwenda kuyamaliza tu, kudai haki yake – uhuru wake. Neno la mwisho ni la Idi.

Alinyanyuka akajipangusa mchanga, na kwa mara nyingine alikwenda kumkabili Idi.

Alimkuta pale pale akilewa pamoja na kile kisura. Aliwatokea bila ya hofu mpaka chini yao, na kwa sauti ngumu yenye ari, pasi na kukitazama kile kisura, akamwambia Idi:

"Ikiwa hunitaki niache!"

"Ha-ha-ha-a!" alicheka Idi, huku akitetemeka. "Hicho ndicho ulichokujaomba? Kwa nini usiniambie wakati ule ule? Nimekuacha! Nimekuacha! Nimekuacha! Haya toka nenda zako!

Bahati alimwona Mwajuma amesimama juu ya vidaraja, mguu mmoja chini na mwingine juu, sahani ya asusa mkononi. Alipokuwa akiyashuhudia yaliyokuwa yakitokea, uso wake aliufanya uwe na hofu na huzuni, na macho yao yalipokutana yalijuana.

"Bado hujaniacha," Bahati alivinjari, akasoga chini ya Idi na kumnyoshea mkono "Nipe shahada yangu na hutaniona tena!"

"Shahada yako, shahada yako! Ksho asubuhi utaipata. Siwezi kupoteza wakati wangu sasa hivi kumtafuta shehe. Kesho asubuhi nitakuletea huko huko … Haya toka!"

Macho ya Bahati yalikuwa ya maji. Alimtazama Mwajuma, halafu kile kisura kilichokuwa kikichekea ushindi, akamwangalia Idi kichwa hata miguu, akageuka na kuyoyoma.

**Maswali:**

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. *(Alama 08)*

(b) Eleza sifa za Bahati kama anavyosaniriwa katika dondoo. *(Alama 04)*

(ch) Tambua mbinu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. *(Alama 06)*

(d) Fafanua maudhui yanayodhihirika katika dondoo hili. *(Alama 06)*

(e) Ni ujumbe gani unaopata kutoka kauli hizi? *(Alama 04)*
  (i) Bahati alitaka kuja juu kutenda alilojia.
  (ii) ...alijizoazoa akakaa na kuegemea shina la mnazi.

(f) Dondoo hili lina mafunzo yapi kwa msomaji? *(Alama 06)*

## SEHEMU B

**VICENT M. TWEYAMBE:** *Baraka za Mama*

**3.** Baraka ni moja wapo ya maudhui katika riwaya, *Baraka za Mama*. Jadili. (*Alama 33*)

**4.** Eleza sifa za wahusika wafuatao kutoka riwaya, *Baraka za Mama*. (*Alama 33*)

(a) Baraka.
(b) Baguma.
(ch) Madikizela.

**K. W. WAMITILA:** *Nguvu ya Sala*

**5.** (a) Eleza namna msanii wa riwaya *Nguvu ya Sala* anavyofaulu kwa kutumia mbinu ya taswira kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. (*Alama 17*)

(b) Chambua sifa za Susan kama anavyowasilishwa katika riwaya, *Nguvu ya Sala*. (*Alama 16*)

**6.** Jadili masuala muhimu yanayowasilishwa katika riwaya, *Nguvu ya Sala*. (*Alama 33*)

## SEHEMU CH

**KEN WALIBORA**: *Kufa Kuzikana*

**7.** Changanua chanzo cha vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya Wakorosho na Wakanju katika riwaya, *Kufa Kuzikana*. (*Alama 33*)

**8.** Mabadiliko ni sehemu ya maisha ya binadamu. Dhihirisha ukweli wa kauli hii ukirejelea riwaya, *Kufa Kuzikana*. (*Alama 33*)

**NDANDA E. ANTONIO**: *Uchungu wa Mwaridi*

**9.** (a) Eleza chanzo cha mgomo wa wafanyakazi katika shamba la maua la mwamba Athi katika riwaya, *Uchungu wa Mwaridi*. (*Alama 17*)

(b) Jadili athari za mgomo wa wafanyakazi katika shamba la maua la mwamba Athi ukirejelea riwaya, *Uchungu wa Mwaridi*. (*Alama 16*)

**10.** Fafanua fani za lugha ambazo mwandishi ametumia kuwasilisha ujumbe katika riwaya, *Uchungu wa Mwaridi*. (*Alama 33*)

## SEHEMU D

**MASEREKA GEORGE BLACK:** *Uhasama Kilimani*

**11.** (a) Kwa nini kulitokea vita kati ya wenyeji wa jimbo la Bwera na ufalme wa Bunyangabo katika riwaya, *Uhasama Kilimani.* (*Alama 17*)

(b) Fafanua athari za vita kati ya wenyeji wa jimbo la Bwera na ufalme wa Bunyangabo katika riwaya, *Uhasama Kilimani.* (*Alama 16*)

**12.** (a) Jadili hatua zinazochukuliwa na Mbaka Lututu kukomboa wenyeji wa Bwera dhidi ya uongozi mbaya wa ufalme wa Bunyangabo katika riwaya, *Uhasama Kilimani.* (*Alama 17*)

(b) Viongozi katika jamii ya leo wanajifunza nini kutokana na hulka za Mbaka Lutututu katika riwaya, *Uhasama Kilimani*? (*Alama 16*)

**WANYENYA WILLY:** *Jitihada Zafua Dafu*

**13.** (a) Jadili sifa za Masombo kama zinavyowasilishwa katika riwaya, *Jitihada Zafua Dafu.* (*Alama 17*)

(b) Vijana wa leo wanajifunza nini kutokana na mhusika Masombo katika riwaya, *Jitihada Zafua Dafu.* (*Alama 16*)

**14.** (a) Jadili sababu za jamii ya Masombo kumchukia katika riwaya, *Jitihada Zafua Dafu.* (*Alama 17*)

(b) Eleza namna wanajamii walivyobadilisha mtazamo wao juu ya mhusika Masombo. (*Alama 16*)



**MWISHO**